Toleo Maalumu

# JARIDA MAALUMU LA USHIRIKA

## UZINDUZI WA BENKI YA USHIRIKA TANZANIA




**USHIRIKA SASA UNA KWENDA VIZURI - MHE. DKT. SAMIA SULUHU HASSAN**



# USHIRIKA SASA UNAKWENDA VIZURI – RAIS DKT. SAMIA




*Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, akizindua Benki ya Ushirika, Jijini Dodoma*

Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, amesema hivi sasa Sekta ya Ushirika unakwenda vizuri kwa kuongeza tija ya Maendeleo katika ustawi wa Wananchi wengi nchini

Rais Mhe.Dkt. Samia amesema hayo wakati wa Uzinduzi wa Benki ya Ushirika uliofanyika Aprili 28, 2025 Jijini Dodoma.

Rais amesema Ushirika sasa una mwelekeo mzuri kutokana na Vyama vya Ushirika kuwa na msukumo chanya wa kuendeleza shughuli za uchumi hadi kufikia hatua ya kuchangia Mtaji wa kuanzisha Benki ya Ushirika ambayo inamilikiwa na Wanaushirika kwa asilimia 51 na Mtaji wa Shillingi Billioni 58. Aidha, Benki hiyo inaanza ikiwa tayari na matawi manne katika mikoa ya Dodoma, Kilimanjaro, Mtwara na Tabora; pamoja na mawakala 58 ambao wanatokana na Vyama Vikuu vya Ushirika nchini.

Mheshimiwa Rais ametoa rai kwa Benki hiyo kuwa chachu ya kuwafikia Wakulima na Wananchi wengi vijijini kupitia mikopo itakayotolewa.

Pamoja na mambo mengine, ameitaka Tume ya Maendeleo ya Ushirika kuendelea kuimarisha usimamizi wa Vyama ili vijiendeshe kibiashara, kutumia Mifumo ya TEHAMA na mahesabu yasomwe kwa wakati.

Uzinduzi huo umehudhuriwa na Viongozi mbalimbali wa Serikali, Wanaushirika, Wadau wa Maendeleo, Taasisi za Kifedha, Wabunge, Vyama vya Siasa pamoja na Wakazi wa Jiji la Dodoma.

**''Ushirika unakwenda vizuri kwa kuongeza tija ya Maendeleo katika ustawi wa Wananchi wengi nchini''**

# NDOTO IMETIMIA UZINDUZI BENKI YA USHIRIKA

Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan amesema kwa muda mrefu Wanaushirika wamehitaji Benki itakayowahudumia moja kwa moja na hatimaye ndoto hiyo imetimia.

Dkt. Samia amesema hayo wakati akizindua Benki ya Ushirika (COOP Bank) jijini Dodoma, Aprili 28, 2025.

Amesema uanzishwaji wa Benki hiyo ni utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya mwaka 2020/25 pamoja na mawazo ya muda mrefu ya uhitaji wa upatikanaji wa mitaji nafuu ya kuwezesha kuongeza tija na uzalishaji wa shughuli za kiuchumi za Ushirika.

Amewataka wanaushirika kutumia fursa za kuanzishwa kwa Benki hiyo kuongeza mitaji na kuchochea kasi ya uendeshaji wa Ushirika nchini kutokana na Wanaushirika kuwa wamiliki wa asilimia 51 wa Benki ambayo inaanzishwa ikiwa na Mtaji wa Millioni 58, Mawakala 58 ambayo ni Vyama vya Ushirika na SACCOS.

“Mna maelfu ya wateja ambao tayari wamejiunga na Benki hii, inatia moyo kuona mmejipanga kuhakikisha kuwa huduma zenu zinafika kwa walengwa wote kwa urahisi na gharama nafuu,” Dkt. Samia



Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, akihutubia Wanaushirika wakati wa Uzinduzi wa Benki ya Ushirika, Jijini Dodoma

Amepongeza hatua hiyo yenye ubunifu wa kutumia Ofisi zote za Vyama vikuu vya Ushirika na SACCOS ili kufikia wananchi wa kipato cha chini na vijijini, wakulima na wafanyabiashara wadogo.

“Natoa rai kwa vyama vya Ushirika kushirikiana na Benki kupanua mtandao wake ili huduma zifike na kupatikana kwa urahisi,” amesema Mhe. Rais

Amesisitiza kuwa pamoja na kwamba benki hii itajikita katika kuhudumia Ushirika na sekta ya kilimo ni ameitaka Benki hiyo kuzingatia misingi ya uendeshaji ya kibishara na kibenki ili iweze kujiendesha kwa uimara na uendelevu wa Benki hiyo.

Ametoa rai kwa mabenki mengine na wadau wa sekta ya fedha kushirikiana na benki hii kutokana na kwamba benki hiyo imeanzishwa kwa malengo ya kuongeza nguvu ya kuhudumia Wananchi wengi hasa vijijini.

Pamoja na mambo mengine Rais ametaka Wakulima na Wanaushirika kuunganishwa na Mifuko ya Hifadhi ya Jamii ili kuwawezesha kuwa na akiba hasa za uzeeni nguvu zinapoisha akisisitiza kuwa huo utakuwa ni ubunifu utakaowasaidia Wakulima pamoja na huduma za Bima ya Afya ili kuongeza ustawi wa Wananchi.

Amesema kwa upande wa Serikali hatua za makusudi nyingi zinaendelea kuimarisha Ushirika kama vile kuimarisha mifumo ya masoko ya mazao ya Wakulima ikiwemo matumizi ya mifumo ya mauzo ya Stakabadhi ya Ghala, TMX pamoja na matumizi

ya TEHAMA ili kuongeza uwazi na kuondoa ubadhilifu. ili kuongeza uwazi na kuondoa ubadhilifu. Hivyo, amewataka Wakulima kutumia fursa hizo kuongeza uzalishaji na tija ya Kilimo kukuza uchumi na Pato la Taifa.




*Wanaushirika wakifuatilia hotuba ya Rais wa Jamhuri ya muungano wa Tanzania, Mhe.Dkt. Samia Suluhu Hassan, katika uzinduzi wa Benki ya Ushirika, Jijini Dodoma.*



*Baadhi ya viongozi wa Tume ya Maendeleo ya Ushirika wakifautilia hotuba ya Rais wa Jamhuri ya muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan katika uzinduzi wa Benki ya Ushirika, Jijini Dodoma.*




Vuna Zaidi!
Pata Mkopo kwa maendeleo ya kilimo


UZINDUZI WA BENKI YA
UZINDUZI WA

# MAGEUZI YA SEKTA YA USHIRIKA KUCHOCHEA UCHUMI– WAZIRI MKUU




*Waziri Mkuu, Mhe. Kassim Majaliwa, akihutubia Wanaushirika wakati wa Kongamano la Ushirika kuelekea uzinduzi wa Benki ya Ushirika, Jijini Dodoma.*

Waziri Mkuu, Mhe. Kassim Majaliwa, amesema Serikali imeendelea na hatua mbalimbali za mageuzi katika sekta ya Ushirika ili kuimarisha uchumi na kuleta maendeleo kwa wananchi wengi nchini.

Waziri Mkuu amesema hayo wakati akifungua kongamano la Ushirika Aprili 27, 2025 ikiwa ni katika kuelekea Uzinduzi wa Benki ya Ushirika uliofanyika Aprili 28,2025, Jijini Dodoma

Waziri Mkuu amebainisha baadhi ya hatua zilizofanyika katika kuimarisha Ushirika ili kuongeza kasi ya kukuza uchumi ni pamoja na kuboresha Mifumo ya Usimamizi ya Ushirika, kuimarisha masoko ya mazao kupitia Stakabadhi za Ghala, upatikanaji wa pembejeo pamoja na uboreshaji wa huduma za fedha ikiwemo kuanzisha Benki ya Ushirika.

Aidha, ametoa wito kwa wadau wa maendeleo na taasisi za kifedha kushirikiana na Benki ya Ushirika ili kuwa sehemu ya mageuzi ya Ushirika yatakayokuwa chachu ya maendeleo ya Wanaushirika na wananchi wengi kupitia kilimo, uvuvi, ufugaji na sekta nyingine za kiuchumi

Mheshimiwa Majaliwa amewataka wakulima na wananchi kwa ujumla wahakikishe wanajiunga na Vyama Vya Ushirika vilivyosajiliwa, ili waweze kunufaika na fursa mbalimbali zinazotolewa na Serikali na wadau wa maendeleo.

“Wadau wote wa maendeleo, endeleeni kushirikiana na Serikali katika kutoa rasilimali, utaalamu na ubunifu unaohitajika ili kuendeleza sekta hii muhimu, Wizara ihakikishe maandiko ya taarifa zilizozinduliwa zinaandaliwa pia kwa lugha ya Kiswahili ili kuwawezesha wananchi wengi zaidi kunufaika nazo.”

Kadhalika, Waziri Mkuu amesema Sekta ya Ushirika nchini inaendelea kuimarika kwa kasi, ikiwa ni mhimili muhimu wa maendeleo ya kiuchumi na kijamii, hasa katika maeneo mbalimbali.

“Hadi sasa, Tanzania inajivunia kuwa na zaidi ya vyama 7,000 vya Ushirika vilivyosajiliwa, vyenye jumla ya wanachama zaidi ya milioni nane. Vyama hivi vinajumuisha sekta mbalimbali za uchumi kama vile kilimo, uvuvi, madini, biashara na huduma za kifedha.”

Waziri wa Kilimo Mhe. Hussein Bashe (Mb), amesema Benki ya Ushirika inamilikiwa na Wanaushirika kwa asilimia 51 jambo ambalo litachangia kuongeza tija katika Ushirika kwa kuwasaidia Wanaushirika kupata mikopo ya kuendesha shughuli zao

kiuchumi kwa kuelewa mahitaji maalum ya Wakulima na Wanaushirika wengine.

Mwenyekiti wa Tume ya Maendeleo ya Ushirika Abdulmajid Nsekela amebainisha kuwa uanzishaji wa Benki ya Ushirika ni utekelezaji wa Vipaumbele vya Tume, ambayo itasaidia kuhudumia sekta mbalimbali na kuleta ujumuishi wa Kifedha na kufikia wananchi wengi.

Shughuli zingine zilizofanyika katika kongamano hilo ni pamoja na uzinduzi wa taarifa ya kilimo ya mwaka 2022/23- 2023/24, utiaji saini wa hati za makubaliano ya mashirikiano ya taasisi mbalimbali na Benki ya Ushirika, utoaji wa tuzo kwa michango na Uwekezaji wa kuhamasisha uanzishaji wa Benki ya Ushirika.



*Waziri Mkuu, Mhe. Kassim Majaliwa, akimkabidhi Tuzo ya Usimamizi Bora wa Sekta ya Ushirika Mrajis na Mtendaji Mkuu wa Tume ya Maendeleo ya Ushirika Dkt. Benson Ndiege wakati wa Kongamano la Ushirika kuelekea Uzinduzi wa Benki ya Ushirika*




*Waziri Mkuu, Mhe. Kassim Majaliwa, akizindua wa Taarifa ya Kilimo ya Mwaka 2022/23 wakati wa Kongamano la Ushirika kuelekea siku ya Uzinduzi ya Benki ya Ushirika, Jijini Dodoma.*

Toleo Maalumu
Uzinduzi wa Benki ya Ushirika

*27 na 28 April, 2025*

# MATUKIO MBALIMBALI WAKATI WA UZINDUZI WA BENKI YA USHIRIKA



*Waziri Mkuu, Mhe. Kassim Majaliwa akipata maelezo kutoka kwa Meneja Mkuu wa Chama Kikuu cha Ushirika WETCU, Samweli Jokea, katika maonesho ya Uzinduzi wa benki ya Ushirika, jijini Dodoma.*




*Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu cha Ushirika Moshi (MoCU), Prof. Alfred Sife, akichangia mjadala wa historia na mchango wa Ushirika katika maendeleo ya nchi.*




*Waziri wa Kilimo, Mhe. Hussein Bashe akimkabidhi Mwenyekiti wa Kamisheni ya Tume ya Maendeleo ya Ushirika, Abdulmajid Nsekela, mfano wa Hundi ya Shilllingi Billioni 5, mchango wa mtaji wa Benki ya Ushirika.*




*Mhe. Rais. Dkt. Samia Suluhu Hassan, akikabidhiwa Tuzo na Waziri wa Kilimo, Mhe. Hussein Bashe kwa mchango wake katika kuanzishwa kwa Benki ya Ushirika.*

# UANZISHWAJI WA BENKI YA USHIRIKA NI UTEKELEZAJI WA ILANI YA CCM – WASIRA

Makamu Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi – CCM bara, Stephen Wasira, amesema uanzishwaji wa benki ya ushirika na maendeleo ya ushirika ni azimio la chama hicho ambayo ni sera ya msingi iliyorithiwa kutoka vyama vya ukombozi vya TANU na Afro Shiraz.

Amesema hayo, 28 Aprili, 2025, wakati wa uzinduzi wa benki ya Ushirika uliofanyika jijini Dodoma akitoa salamu za pongezi kutokana na uanzishwaji wa benki hiyo kwa wanaushirika.

“Chama cha mapinuzi kinaendeleza sera hii, kwa imani ya kwamba shabaha ya maendeleo ni kumkomboa mwanadamu kwa kazi anayoifanya lakini Ushirika unamwezesha kwa kushirikiana na wenzake kufanya mambo ambayo kwa mtu mmoja mmoja hawezi kufanya, kama kuagiza mbolea” alisema Wasira.

Aliongeza kuwa,Chama Cha Mapinduzi kinaamini kumkomboa mwanadamu kiuchumi kupitia Ushirika, hakuna namna nyingine ya watu hawa ya kupiga hatua kiuchumi bila kushirikiana.

Aidha, kazi inayofanywa na Serikali ya kuboresha maendeleo ya Ushirika nchini ili kuboresha maisha ya watanzania kupitia ushirika ni kutimiza Ilani ya chama hicho.



*Makamu Mwenyekiti wa CCM, Bara, Stephen Wasira akizungumza na wanaushirika katika Uzinduzi wa Benki ya Ushirika, Jijini Dodoma*

“Kwahiyo tunakuja hapa, kuona kazi inayofanywa na serikali kuwa ni azimio la Chama Cha Mapinduzi la kuwafanya watanzania wote wawe na maisha bora ya kiuchumi kutoka siku hadi siku”,

“Kazi kubwa ya chama chetu na agenda yake ambayo haina kikomo ni kuboresha maisha maisha ya watu wake ili maisha ya leo yawe bora kuliko jana na kesho yawe bora kuliko leo”, alisema Wasira

Benki ya ushirika Tanzania ilizinduliwa na Rais wa Jamhuri ya muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassani, ambapo kuanzishwa kwa benki hiyo ni hatua muhimu za kuimarisha ushirika nchini Tanzania.

**KWA HABARI, TAARIFA NA MATANGAZO MBALIMBALI KUHUSU USHIRIKA TEMBELEA KURASA ZETU ZA KIJAMII**

**Instagram: ushirika_tcdc**
**Facebook: Tume ya maendeleo ya Ushirika**
**Youtube: Ushirika TV**
**Tovuti: www.ushirika.go.tz**

# USHIRIKA UNA MCHANGO MKUBWA KATIKA UKOMBOZI WA TAIFA - Prof. Kabudi



*Waziri wa Habari , Utamaduni, Sanaa na Michezo, Mhe. Prof. Palamagamba Kabudi, akiongoza mjadala wa Wataalamu kujadili historia na mchango wa Ushirika nchini*

Vyama vya Ushirika hapa nchini ni miongoni mwa Wadau muhimu walioshiriki katika mapambano ya uhuru hapa nchini kutokana na nguvu ya ushawishi iliyokuwepo kiuchumi na kisiasa.

Historia ya Vyama Vya Ushirika inaonesha ilianza mwaka 1925 ambapo chama cha Ushirika, Kilimanjaro
Native Cooperative Society (KNCU) kilichopo Mkoani Kilimanjaro kilianzishwa na Wakulima wa Kahawa kwaajili ya Maslahi yao ikiwemo huduma za Pembejeo, masoko na mikopo.

Waziri wa Utamaduni Sanaa na Michezo, Prof. Palamagamba Kabudi katika Kongamano la uzinduzi wa alisema Viongozi wa Ushirika ni miongoni mwa watu waliotoa mchango mkubwa wa kudai Uhuru wa Tanganyika.

"Baadhi ya Viongozi wa Vyama hivi vya Ushirika walikuwa ni Viongozi wa Chama cha TANU, ambao walitumia muunganiko wa wakulima katika vyama vya ushirika kujenga nguvu ya umoja kwenye kudai uhuru," alisema Prof. Kabudi.

Vyama vya Ushirika viliendelea kushamiri na hadi maeneo mengine ya kanda ya ziwa vikiongozwa na Chama Kikuu cha Ushirika (Victoria Federation of Cooperative Union), Chama cha Ushirika katika Mkoa wa Kagera Bukoba Bahaya Union hadi Ruvuma Chama cha Ngoni Matengo Cooperative Union.

Viongozi wa Ushirika walioshiriki michakato ya kudai Uhuru wa Tanganyika wakiongozwa na Hayati Mwl. Julius Kambarage Nyerere ambaye aliunga mkono jitihada za Ushirika kutokana na kuhamasisha msingi wa falsafa ya Ujamaa na kujitegemea iliyolenga kujikwamua kiuchumi.

Aidha, viongozi hao walioshiriki katika harakati hizo za ukombozi ni pamoja na Sir George Kahama, Paul Bomani, Ndugu Jeremiah Kasambala na Ndugu John Mhvaile walitumia Ushirika kama njia ya Kisiasa na Uchumi

Prof. Kabudi anabainisha kuwa



*Waziri wa Utamaduni Sanaa na Michezo, Prof. Palamagamba Kabudi, akichangia mada katika Kongamano la Ushirika kuelekea Uzinduzi wa Benki ya Ushirika Jijini Dodoma.*

Ushirika uliendelea kushamiri baada ya Tanganyika kupata Uhuru mwaka 1961; na baadaye mwaka 1976 kupata changamoto za kiuendeshaji na kusababisha kuzorota kwa Vyama vya Ushirika nchini kulikotokana na ubadhilifu uliopelekea Vyama kufutwa.

"Katika makosa yote yaliyowahi kutokea tumejifunza umuhimu wa Ushirika na kwamba Vyama vya Ushirika havina mbadala katika kujenga uchumi, Uchumi wa Ushirika unahitaji Mtaji mkubwa hasa wa mikopo ya muda wa kati na muda mrefu," alisema prof. Kabudi

Akibainisha kuwa majibu ya mahitaji hayo ni kuanzishwa kwa Benki ya Ushirika yenye kumilikiwa na Wanaushirika kwa asilimia kubwa, Serikali, Sekta binafsi na wanahisa wengine wakiwemo wanahisa wa kimkakati hasa Benki za Ushirika kutoka katika mataifa yaliyofanikiwa.

Dhamira ya Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan inaenda sambamba na dhamira za awali za kuinua hali za Maisha ya Wananchi kwa kuimarisha vipato vyao kupitia Ushirika.

Dhamira hii inabainishwa wazi na Mhe. Rais katika Mkutano na Wanaushirika pamoja na Maafisa Ugani Agosti, 2024 Jijini Dodoma akieleza nia ya kurejesha Hadhi ya Ushirika nchini.



*Wanaushirika wakifuatilia hotuba ya Waziri Mkuu katika kongamano la Ushirika, Jijini Dodoma.*

"Tunataka kurejesha Hadhi ya Ushirika nchini, Ushirika uendeshwe kisasa, uwekezaji ufanywe kitaalamu ukiwa na lengo la kumnufaisha moja kwa moja Mwanaushirika," amesema Mhe. Dkt. Samia.

**"Baadhi ya Viongozi wa Vyama hivi vya Ushirika walikuwa ni Viongozi wa Chama cha TANU, ambao walitumia muunganiko wa wakulima katika vyama vya ushirika kujenga nguvu ya umoja kwenye kudai uhuru," alisema Prof. Kabudi.**

# VYAMA VYA USHIRIKA VINA MCHANGO KWA UCHUMI WA TANZANIA – DKT. BASHIRU




*Mbunge na Katibu Mkuu Mstaafu wa CCM, Mhe. Dkt. Bashiru Ally, akizungumza katika kongamano kuelekea Uazinduzi wa Benki ya Ushirika, Jijini Dodoma.*

Mbunge na Katibu Mkuu mstaafu wa CCM, Mhe. Dkt. Bashiru Ally, amesema Ushirika una changia kwa kiasi kikubwa maendelo ya uchumi wa Tanzania kutokana na kuimarishwa kwa sekta hiyo chini ya Tume ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania.

Ameeleza hayo, 27 Aprili, 2025, wakati wa siku ya kwanza ya uzinduzi wa Benki ya Ushirika uliofanyika jijini Dodoma akitoa salamu na pongezi kutokana na uanzishwaji wa benki hiyo kwa wanaushirika.

Aliongeza kuwa, ili ushirika uweze kufika mbali inapaswa kuepuka makosa yaliyofanywa zamani ya kufuta Vyama vya Ushirika kwani uligharimu Sekta ya Ushirika kwa kiasi kikubwa.

Aidha, alishauri ni vyema kabla ya kuvunja au kufuta ni lazima utafiti na uchunguzi wakina ufanywe kabla kufikia maamuzi ya kufuta Ushirika kwani kufuta ni rahisi na kuanzisha upya ni gharama zaidi.

Pia, alisema kazi inayofanywa na Serikali ya kuboresha Ushirika nchini inalenga kuimarisha uchumi maisha ya Wanaushirika.

"Kwahiyo niwaombe sana viongozi wa Ushirika muwe waadilifu mfanye kazi kwa kufuata sheria, kanuni na taratibu, lasivyo historia itajirudia na itakuwa ni aibu kwa Taifa Serikali imeweka Billioni 5 hapo mkiua hiyo Benki mtakuwa mmeikosea sana Serikali yetu"alisema Dkt. Bashiru amesema watu wote wanajua kuwa Sekta ya Kilimo ni uti wa mgongo wa uchumi wa Taifa na Kilimo ndiyo kitovu cha Vyama Vya Ushirika na kwa awamu hii ya Uongozi umefanya mageuzi makubwa kwa lengo la kuongeza mchango wa Ushirika katika uchumi ili uweze kusaidia wananchi kwani Ushirika ni sekta inayomgusa mwananchi moja kwa moja.

"Ni matumaini yangu kwamba Vyama vya Ushirika vitafanya kazi ya kumhudumia Mkulima na vitakuwa chini ya usimamizi wa wakulima wenyewe na ndiyo maana Benki ya Ushirika mmiliki wake Mkuu ni wanaushirika wenyewe hii inaleta nguvu ya kutunza kilichopo kwasababu inakuwa ni mali yenu" Dkt. Bashiru

Vilevile zipo taasisi nyingi ambazo zinafanya kazi na Tume ya Maendeleo ya Ushirika kwa karibu, vyombo hivi vikiamua kufanya kazi kwa kushirikiana na maelewano kwa kuzingatia maslahi ya Taifa na maslahi ya wakulima Ushirika utazidi kusonga mbele kwasababu kutakuwa na kundi kubwa linalomlinda na kumtetea mkulima.

Dkt. Bashiru amesema, kuna haja ya kuwa na mitaji na vyanzo vya fedha kwaajili ya maendeleo ya Sekta ya Ushirika na pia sekta za fedha kuwekeza kwenye Ushirika ili kurahisiaha upatikanaji wa mitaji na kukuza Ushirika.

"Na ndiyo maana tunaona Serikali imewekeza shilingi Billioni 5 katika mchakato wa kuanzisha Benki ya Ushirika Tanzania hii inazidi kuimarisha Sekta ya Ushirika na kuwezesha wakulima kupata huduma bora za kifedha, niwakumbushe tu tunzeni benki hii kwani ni mali yenu wanaushirika," amesema Dkt. Bashiru

Benki ya Ushirika Tanzania ilizinduliwa 28, Aprili na Rais wa Jamhuri ya muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Benki hii inakwenda kuwa mkombozi kwa wanaushirika nchini.



Wanaushirika wakifuatilia hotuba ya Waziri Mkuu katika kongamano la Ushirika, Jijini Dodoma.

# VIONGOZI WA USHIRIKA WAPONGEZWA KWA USIMAMIZI BORA WA USHIRIKA



Waziri wa Kilimo, Mhe. Hussein Bashe, akizungumza katika kongamano la Ushrika, Jijini Dodoma.

Waziri wa Kilimo, Mhe. Hussein Bashe, amepongeza viongozi wa vyama vya Ushirika kwa kufanya mapinduzi katika Ushirika kutokana na kuongezeka mauzo ya mazao ya wakulima kupitia Ushirika kwa misimu miwili kati ya mwaka 2023/2024 na 20224/2025.

Ametoa pongezi hizo Aprili 27, 2025 katika kongamano la uzinduzi wa benki ya uliofanyika jijini Dodoma ikiwa ni sehemu ya kuimarisha Maendeleo ya Ushirika nchini.
Amesema, mauzo ya mazao kupitia mifumo ya Stakabadhi za ghala na TMX kwa misimu miwili umeongezeka ambapo 2023/2024 vyama vya ushirika viliuza mazao kilo milioni 1.6 zenye thamani ya Shilingi Trilioni 1.9 hadi kufikia tani 2.2 yenye thamani ya Shilingi. Trilioni 4.2 kwa msimu wa mwaka 20224/2025.

"Mauzo ya mazao kupitia ushirika umeongezeka sana, nawashukuru sana viongozi wa Ushirika kwa kusimamia vizuri Ushirika" alisema Bashe.

Aidha, amesistiza kuwa Benki ya Ushirika ni kwa ajili ya wanaushirika ambapo wanaomiliki hisa asilimia 51, Serikali asilimia 10 na wadau wengine asilimia 39 hivyo waitumie vyema kwa maendeleo yao.

# BENKI YA USHIRIKA KUWAFIKIA WANANCHI WENGI - NG`URAH



*Mkurugenzi Mkuu wa Benki ya Ushirika Tanzania, Godfrey Ng'urah , akizungumza na wanaushirika katika uzinduzi wa Benki hiyo Jijini Dodoma*

Mkurugenzi Mkuu wa Benki ya Ushirika Tanzania Godfrey Ng'urah amesema Benki ya Ushirika ni Benki itakayoleta muelekeo chanya wa maendeleo kupitia wigo na miundo mbinu ya utoaji huduma ikiwemo mtandao wa mawakala wa vyama vikuu vya Ushirika vipatavyo 58 kote nchini.

Akiongea katika uzinduzi wa Benki ya Ushirika Aprili 28, 2025 Mkurugenzi Ng'urah amebainisha kuwa katika kuhakikisha kuwa Benki hiyo inawafikia na kutoa huduma kwa Wananchi wengi tayari imeanza na matawi manne ya Moshi, Tabora, Mtwara na Dodoma na ikitarajia kuongeza matawi mengi zaidi ili kupanua huduma za Kifedha kwa Wanaushirika na wananchi wengi.

" Benki itajipanua kimkakati kwa kutumia muundo wa vyama vya vya ushirika kama mawakala wake ili wanaushirika waweze kupata huduma zake ikiwa ni pamoja na akaunti za kilimo Tija kwa wakulima isiyo na gharama yoyote ya uendeshaji ili wakulima awe na akiba isiyokatwa kwenye benki," amesema

Aidha, amesema kutokana na ubunifu na azma ya kwenda na huduma za kisasa hata kwa wateja wanaokuwa mbali na matawi ya Benki wanaweza kupata huduma kupitia bidhaa mahusisi kama vile Huduma za kibenki mkononi -Coop Pesa, huduma za Intaneti - COOP NET, bidhaa kwa watoto, bidhaa kwa wajasiriamali (Jasiri Akaunti) na Bima kwa wakulima pamoja na Ghalapesa.



Mkurugenzi Ng'urah amebainisha kuwa matarajio ya benki hiyo ni kuleta matokeo chanya ya huduma za Benki kwa Vyama vya Ushirika na makundi maalum ya kijamii ziwafikie wanaushirika na sekta binafsi, walio nje ya mfumo rasmi wa kifedha kote nchini.

" Muelekeo wa Benki yetu ni kuleta Ujumuishi wa Kifedha (Financial inclusion) kwa makundi ya wakulima na wajasiriamali walio nje ya mfumo wa fedha, fursa za kibiashara ndani na nje ya sekta, na Masoko endelevu kwa sekta ya Ushirika nchini na kuwafikia watanzania wasipungua milioni 10 ifikapo, mwaka 2030," amesema.

# BENKI YA USHIRIKA TANZANIA (COOP BANK)




*Limetolewa na*
*Tume ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania (TCDC)*
*Mtaa wa Kuu, S. L. P. 201, DODOMA*
*Simu: +255262322456, Telefax: +255262321973*
*Barua Pepe: ushirika@ushirika.go.tz Tovuti: www. ushirika.*